# WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

## JARIDA LA MTANDAONI - SEPTEMBA 2023



Limeandaliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara | www.mit.go.tz

Viwandabiashara



# Wawekezaji kuhudumiwa kupitia Dirisha Moja la Huduma

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameitaka Idara ya Kazi, Ofisi ya Waziri Mkuu kusimamia mpango wa urithishwaji wa ujuzi kwa wazawa kama ilivyobainishwa katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini.

Rais Samia ametoa tamko hilo Septemba 20, 2023 mara baada ya ufunguzi wa kiwanda cha kutengeneza vioo cha Sapphire Float Glass.

Aidha, Rais Samia amesema mpango huu utawasaidia Watanzania wengi kupata ujuzi na ajira na kumsaidia mwekezaji kupunguza gharama za kuajiri wataalamu wa kigeni.

Vile vile, Rais Samia amesema Serikali inaendelea kuwekeza kwenye mifumo ya utoaji huduma ili kupunguza urasimu na kutekeleza hatua za kiuchumi ambazo zimepokelewa vyema na wadau wa maendeleo.

Hali kadhalika, Rais Samia amesema Serikali inatarajia kuzindua Mfumo wa kielektroniki wa kuhudumia wawekezaji (Tanzania Electronic Investment Window) ambao utaunganisha taasisi 12 za Serikali zinazotoa huduma kwa wawekezaji.

Rais Samia pia amesema wawekezaji watakaotaka kuwekeza chini watapewa msaada katika mchakato wa usajili wa kampuni, upatikanaji wa ardhi, vibali na leseni kupitia dirisha moja la huduma ndani ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Rais Samia amehitimisha ziara yake mikoa ya kusini ambapo akiwa njiani kurejea jijini Dares Salaam amezungumza na Wananchi wa Somanga, Ikwiriri na Mkuranga na kuwaeleza nia ya Serikali ya kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo.

# Tanzania Yazindua Kiwanda Kikubwa cha Vioo Afrika Mashariki na Kati



Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (MB) amesema uzinduzi wa kiwanda kikubwa cha vioo Afrika Mashariki na Kati ni hatua muhimu katika kuendeleza sekta ya viwanda Nchini Tanzania.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Septemba 20, 2023 Mkuranga, Pwani, Waziri Kijaji amesema uzinduzi wa Kiwanda hicho moja wapo wa viwanda vinne vya kutengeneza vioo Barani Afrika ni ushindi mkubwa kwa Tanzania kwa kuongeza uzalishaji wa bidhaa za viwandani nchini.

Aidha, ametoa wito kwa wananchi kuchangamkia fursa za ajira zinazotolewa na Kiwanda cha Sapphire chenye uwezo wa kuzalisha tani 400,000 za vioo kwa mwaka na kinatarajiwa kutoa ajira za moja kwa moja 1,650 na zisizo za moja kwa moja 6,000.

Pia, amebainisha kuwa Kiwanda hicho kinatarajiwa kutumia malighafi zinazopatikana na Nchini Tanzania, ikiwa ni pamoja na dolomite, silca sand, limestone, feldspar pamoja na magadi soda yanayopatikana Engaruka na kinatarajia kuuza bidhaa zake katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Serikali ya Awamu ya Sita ina dhamira ya dhati ya kuendeleza sekta ya viwanda nchini," alisema Waziri Kijaji. "Tutaendelea kutoa mazingira mazuri kwa wawekezaji ili waweze kuwekeza nchini Tanzania."

# HABARI PICHA : UZINDUZI WA KIWANDA CHA VIOO CHA SAPPHIRE MKURANGA










# RAIS SAMIA AKISHIRIKI MAJADILIANO KUHUSU MIFUMO YA CHAKULA AFRIKA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa katika majadiliano ya Wakuu wa Nchi kuhusu mifumo ya chakula barani Afrika Septemba 7, 2023 wakati wa Kongamani la Mifumo ya Chakula (AGRF) uliofanyia katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC). Kongamano hilo lililowahusisha Wakuu wa Nchi lililowakutanisha Marais wa tano (5) kutoka Afrika ambao ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Kenya, Mhe. William Ruto, Rais wa Burundi, Mhe. Evarist Ndayishimiye, Rais wa Senegal Mhe. Macky Sall pamoja na Rais wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi wakizungumzia fursa, changamoto na mikakati ya Nchi za Afrika katika kukuza na kuendeleza sekta ya chakula



Viongozi mbalimbali pamoja na wadau wa Kilimo wakiwa kwenye Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) uliofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) tarehe 07 Septemba, 2023.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akihutubia wakati wa Ufunguzi wa Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika kwa Mwaka 2023(AGRF) katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere Jijini Dar es salaam. Tarehe 05 Septemba 2023.

# Tanzania Kuimarisha Mifumo ya Chakula

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ametaja namna ambavyo Tanzania imedhamiria kufikia lengo namba mbili la umoja wa mataifa (SDG2) linalohusu kuufikia ulimwengu usio na njaa mwaka 2030.

Akizungumza katika ufunguzi wa Kongamano la Mifumo ya Chakula (AGRF) lililofanyika jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa (JNICC) Dkt. Mpango amesema Kongamano hilo utainufaisha Tanzania kuimarisha mifumo ya chakula kwa kuwekeza zaidi kwenye rasilimali ardhi na nguvu kazi ya wanawake barani Afrika.

Amesema Tanzania inajivunia jitihada za maboresho ya mifumo ya chakula na imejitoa kushirikiana na wengine ambapo lengo kuu ni kuwa na ulimwengu usio na njaa ifikapo mwaka 2030.

Akitoa mifano ya namna Tanzania imeweka jitihada kwenye suala hilo Dkt. Mpango amesema, hivi sasa kilimo hapa nchini kinatambulika kama chanzo kikuu cha ukuaji wa uchumi ambapo kimetoa ajira kwa zaidi ya asilimia 65 ya wananchi huku kikichangia katika pato la Taifa kwa asilimia 27 Tanzania Bara na asilimia 21 kwa Zanzibar.

Amesema sekta ya kilimo inachangia katika usafirishaji wa bidhaa zake nje ya nchikwa zaidi ya asilimia 30 na kuzalisha asilimia 65 za malighafi kwa ajili ya viwanda vya Tanzania.






# Afrika Kishirikiana kutatua changamoto ya usafirishaji bidhaa baina ya nchi

Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.) amesema Nchi za Afrika zimekubaliana kushirikiana katika kutatua changamoto mbalimbali za kibiashara ikiwemo usafirishaji wa bidhaa ndani ya Bara la Afrika ili kuiwezesha Sekta Binafsi ambayo ni injini ya ujenzi wa uchumi kufanya biashara kwa ufanisi.

Waziri Kijaji ameyasema hayo Septemba 06, 2023 wakati akishiriki Mkutano wa Watendaji Wakuu wanaohusika na Sekta ya Biashara na Uwekezaji wakati wa Kongamano la Mifumo ya Chakula (AGRF) kwa mwaka 2023 lililofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam.

"Kupitia AGRF, tumekubaliana kuanza kushughulikia changamoto kubwa zilizopo ikiwemo gharama kubwa za usafiri na usafirishaji bidhaa ndani ya bara letu na muda mrefu wa kusafiri kutoka nchi moja ya Afrika kwenda nchi nyingine". Amesema Dkt. Kijaji.

Vilevile, amebainisha kuwa nchi hizo za Afrika zimekubaliana kila moja kuwekeza ndani ya nchi yake na kushirikiana na nchi nyingine hususani katika usafiri wa ndege za mizigo ili ziweze kusafiri zaidi ndani ya Bara la Afrika na kufikia lengo la kufanya biashara kwa pamoja na kwa haraka.

Dkt. Kijaji amempongeza Rais wa Jamhuri ya Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ununuzi wa ndege ya mizigo ambayo itaanza kupunguza muda wa kusafirisha mizigo kutoka nchi moj ya Afrika kwenda nchi nyingine.

Dkt. Kijaji pia amesema katika kutatua changamoto hiyo Tanzania imeridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya SADC ya 2012 yenye dhamira ya kuondoa changamoto wanazokumbana nazo wafanyabiashara nchini wanaposafirisha bidhaa kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine.

Vilevile, amebainisha kuwa Tanzania imeanza utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA) ambapo imeanza kushirikiana na mataifa ya Afrika kuhakikisha miundombinu ya ufanyaji biashara inawekezwa nchini na bidhaa ya kwanza ya Kahawa iliuzwa kutoka Tanzania kwenda Senegal kupitia Mkataba huo.





# Uhusiano kati ya Tanzania na China ni kichocheo cha Uwekezaji





Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Kassim Majaliwa ametoa rai kwa wawekezaji kutoka China kuja kuwekeza Nchini kwa kuwa na uhusiano kati ya Tanzania na China ni Kichocheo cha uwekezaji.

Waziri Mkuu Majaliwa ameyasema hayo Septemba 25, 2023 Dar-Es-Salaam alipokuwa akifunga Mkutano wa uwekezaji kati ya Tanzania na China .

Kauli ya Majaliwa imekuja wakati uwekezaii wa China ukiongezeka na kuifanya nchi hivo kuongoza nchi zinazowekeza zaidi Nchini.

“Takwimu kuanzia mwaka 1997 hadi 2023 zinaonyesha China inaongoza uwekezaji uliofikia zaidi ya dola 10 bilioni pamoja na Jumla ya Miradi 1,134 ya China imesajiliwa katika Kituo cha Uwekezaji (TIC) ambayo inachangia kutoa ajira nchini.” Amesema Waziri Mkuu.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji Mhe. Prof. Kitila Mkumbo akiwa na Naibu Waziri Wizara ya Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe Septemba 25, 2023 walipotembelea Kongani ya Viwanda “Sino- Tan Industrial Park” iliyopo Kwala, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha.

lengo la ziara hiyo ni kuwaleta wawekezaji kuona maeneo ya kuwekeza viwanda vyao katika eneo hilo linaloendelea na ujenzi. Aidha Kongani hiyo inatarajiwa kuwa na Viwanda takribani 200 ambavyo vitajikita katika uzalishaji bidhaa za ngozi, nguo na mavazi, usindikaji wa chakula, madawa, kemikali, nondo na vyuma pamoja na Vifaa vya ujenzi.

# TBS Ongezeni Wigo wa Utoaji Huduma Kikanda nchini

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo imelipongeza Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa utendaji kazi mzuri na kuliagiza kupanua wigo wa utoaji wa huduma za viwango na ubora kwa kuanzisha maabara kikanda nchini ili kuwarahisishia wafanyabiashara kupata huduma hizo kwa urahisi na kuwawezesha kushindana katika soko la ndani na nje ya nchi.

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Mariam Ditopile (Mb.) Septemba 09, 2023 wakati Kamati hiyo ilipotembelea Shirika la Viwango Tanzania (TBS) jijini Dar es Salaam ili kupata elimu kuhusu majukumbu mbalimbali inayoyatekekeza. Aidha, Mwenyekiti wa Kamati hiyo ameipongeza Serikali na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kusimamia uwekezaji wa Maabara za kisasa na viwango vinavyohitajika kimataifa ili kuwawezesha walaji kupata huduma na bidhaa bora zenye usalama pamoja na udhibiti wa bidhaa bandia zinazoingizwa nchini.

Aidha, Wajumbe wa Kamati hiyo walipata fursa ya kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha utoaji wa huduma za viwango na ubora kwa wafanyabiashara wadogo, wakati na wakubwa ili kuwawezesha wafanyabiashara hao kushindana katika soko la ndani na nje ya nchi na kuhakikisha Walaji wanapata bidhaa na huduma bora na salama kwa afya zao na maisha yao kwa ujumla.

Naye Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb.) ameihakikishia Kamati hiyo kuwa Wizara yake itayafanyia kazi maoni na mapendekezo hayo ikiwemo kupitia na kurekebisha Sera, Sheria na Mikakati inayohusiana na Sekta ya Viwanda na Biashara ili kuhakikisha huduma za viwango na ubora zinazotolewa na TBS zinaendana na wakati na mabadiliko ya teknolojia.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TBS Dkt. Athuman Yusuf Ngenya amesema TBS ina jukukumu la kuandaa viwango na kusimamia ubora wa bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini na zile zinazotoka nje ya nchi ili kuhakikisha bidhaa zote zinazoingizwa sokoni zinakidhi matakwa ya viwango ili kulinda afya, usalama na nakuziwezesha kushindana katika soko la ndani na la kimataifa, hivyo kuchochea maendeleo ya uchumi.














# Tunzeni Chakula cha Kutosha na uzeni ziada

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt Ashatu Kijaji (Mb.) amewasihi Watanzania kuuza ziada ya chalula na kubakisha chakula chakutosha hadi msimu ujao ili kutokununua chakula hicho kwa bei kubwa zaidi wakati ujao.

Vilevile, amewashauri Wafanyabiashara wa nafaka kununua nafaka kwa wingi zinapopatikana na kuzisambaza kwenye maeneo zinapohitajika ili kuwasaidia wananchi kununua chakula mapema kwa bei nafuu ukilinganisha na miezi ijayo ya msimu wa kilimo.

Waziri Kijaji ameyasema hayo akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Malima, Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Lugano Wilson na Katibu Tawala wa Mkoa huo Kamishna Dkt. Mussa Ali Mussa alipokuwa akitoa Taarifa ya Tathimini ya Mwenendo wa Bei za Bidhaa Muhimu Nchini kwa Mwezi Septemba 2023 katika Mkutano wa Waandishi wa Habari uliofanyika Mkoani Morogoro 15/09/2023.

Aidha, Waziri Kijaji ametoa rai kwa wazalishaji wa bidhaa zote za viwandani kuongeza jitihada za kuzalisha bidhaa kwa kuzingatia ubora unaohitajika sokoni na kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa ili kukabiliana na kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali nchini.

Vilevile, Waziri Kijaji amebainisha kuwa mwenendo wa bei za bidhaa muhimu kwa Septemba 2023 umeonesha bei ya mazao ya mahindi, unga wa mahindi, maharage, unga wa ngano imepungua, viazi mviringo na sukari himilivu, mafuta ya kupikia na mchele imeongezeka kidogo, wakati bei ya vifaa vya ujenzi kama saruji, nondo na bati imeongezeka kidogo.

Aidha, amewatahadharisha wafanyabiashara kuwa makini na kujiridhisha kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania(TANTRADE) kuhusu Makampuni ya Wakala wanatoa matangazo ya kuandaa safari za kibiashara nje ya nchi bila kufuata taratibu na kuwalaghai kutoa kiasi cha fedha kama sehemu ya gharama za kujisajili ili waweze kushiriki katika ziara hizo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Malima amewashauri wakulima na wazalishaji nchini, kuutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ili waweze kupata manufaa na kuongeza tija ya mauzo ya mazao na bidhaa zao kila Mkoa Nchini.

# Trekta za URUSUS ni nzima zinafanyakazi zinahitaji matunzo

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji ameridhishwa na ubora wa utendaji kazi wa Matrekta yaliyonunuliwa na Serikali maarufu kama URSUS baada ya kuona trekta likilima shamba la Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) Mkoani Morogoro, Septemba 15, 2023. Chuo cha SUA kilinunua Trekta za URSUS 10 kutoka Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) kwa lengo la kutoa mafunzo ya kilimo kwa wanafunzi katika Chuo hicho. Matrekta yote 10 yanafanya kazi hadi sasa. Chuo cha SUA kina Wataalamu wenye uwezo wa kutoa mafunzo ya kiufundi na kufanya matengenezo ya nyenzo zote za kilimo, yakiwemo matrekta.





Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) akiwa na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Eng. Dkt. Lugano Wilson na Mkurugenzi Mwendeshaji wa NDC wakiangalia matengenezo Trekta za URSUS na kuongea na Wataalamu wanaotengeneza trekta hizo katika gereji ndani ya Chuo cha Kilimo Sokoine (SUA) Septemba 15, 2023 Mkoni Morogoro.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), akikagua Trekta aina ya URSUS likilima shamba la Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) Mkoani Morogoro, Septemba 15, 2023.





# Tanzania na Uturuki waimarisha uhusiano wa kibiashara




Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Ashatu Kijaji (Mb.) alisema Tanzania na Uturuki zimeendelea kuimarisha uhusiano wa kibiashara ambao umekuwa ukiongezeka kwa kasi kubwa ambapo wafanyabiashara baina ya mataifa hayo wamekuwa wakifanya biashara yenye thamani kubwa katika sekta mbalimbali nchini ikiwemo ujenzi wa miundombinu.

Waziri Kijaji aliyasema hayo Septemba 19, 2023 akiwa na Balozi wa Uturuki nchini, Dkt. Mehmet Gulluoglu walipofungua Mkutano wa Biashara (B2B) kati ya Tanzania na Uturuki uliofanyika jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuimarisha uhusiano wa biashara kati ya nchi hizo mbili.

Aidha, alitoa wito kwa wafanyabiashara wa kitanzania walioshiriki Mkutano ambao utaongeza chachu ya biashara kwa kutumia fursa mbalimbali zinazopatikana baina ya mataifa hayo mawili katika kukuza na kuendeleza biashara zao na kujipima baada ya miezi sita (6) kuwa bidhaa ngapi zimeuzwa na ngapi zimepokelewa kutoka uturuki.

Aidha, Waziri Kijaji alibainisha kuwa mauzo ya bidhaa kutoka Uturuki kwenda Tanzania yameongezeka kwa kiwango cha wastani wa asilimia 17.3 katika kipindi cha miaka 26 iliyopita kutoka Dola za Marekani milioni 4.55 mwaka 1995 na kufikia Dola za Marekani milioni 500 mwaka 2022.



Vilevile, alibainisha kuwa mwaka 2021, Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 37.6 nchini Uturuki na bidhaa kubwa ilikuwa dhahabu ambayo ilikuwa Dola milioni 14.9 na tumbaku ghafi Dola za Marekani milioni 11.2.



Naye, Balozi wa Uturuki nchini, Mhe. Dkt. Mehmet Gulluoglu alisema wafanyabiashara kutoka kampuni 30 za uturuki katika sekta mbalimbali zikiwemo teknolojia, ujenzi na utengenezaji wa nguo zimekuja kutafuta fursa mbalimbali za uwekezaji na ubia na wawekezaji watanzania wanaowakilishwa na kampuni 100.

“Tanzania na Utururi hatushindani kibiashara bali ni washirika ambao tumekuwa tukisaidiana kwenye kuimarisha biashara mbalimbali kwa watanzania kupeleka bidhaa uturuki na Uturuki kuleta bidhaa hapa Tanzania,” Alisema Balozi Gulluoglu.

# HABARI PICHA




## China

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji(Mb.) amekutana na kufanya mazungumzo kuhusu kuendeleza uhusiano wa kibiashara na China hususan katika uchakataji wa mazao ya kilimo na Balozi wa China nchini, Mhe. Chen Mingjian katika Ofisi Ndogo za Wizara Jijini Dar es Salaam Septemba 11, 2023. Tanzania inasafirisha mazao ya kilimo kama parachichi, kahawa, mahindi , ufuta na asali kwenda China.




## Uturuki

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.) amekutana na kufanya mazungumzo kuhusu kuendeleza ushirikiano wa kibiashara na uwekezaji baina ya Tanzania na Uturuki hususan katika sekta ya kilimo katika mazao ya Chai, matunda na mazao ya misitu kama mbao pamoja na upatikanaji wa soko la bidhaa za Tanzania na Balozi wa Uturuki nchini Mhe. Dkt. Mehmet Güllüoğlu Septemba 11, 2023 katika Ofisi ndogo za Wizara, jijini Dar es Salaam




## Indonesia

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.) amekutana na kufanya mazungumzo kuhusu kuendeleza ushirikiano wa kibiashara baina ya Tanzania na Indonesia na Balozi wa Indonesia nchini Mhe. Tri Yogo Jatmiko Septemba 11, 2023 katika Ofisi ndogo za Wizara, jijini Dar es Salaam. Waziri Kijaji amemhakikishia Balozi huyo kuwa Tanzania iko tayali kuendeleza ushirikiani baina ya nchi hizo na iko tayari kuwezesha miradi ya uwekezaji hususani katika sekta ya kilimo hasa katika uongezaji wa mnyororo wa thamani katika mazao ambayo nchi hiyo imepanga kuyaendeleza kama vile karafuu ili kuongeza ajira na kipato kwa watanzania.




# Wakuu Wamikoa watakiwa kufanya Maonesho ya Utalii

Naibu waziri wa Viwanda na Biashara Mhe Exaud Kigahe (Mb.)amewataka Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania kuhakikisha wanafanya Maonesho ya Utalii ili kukuza utalii na kuongeza mapato ya nchi kwa kuwa sekta hiyo inachangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa.

Kigahe ameyasema hayo Septemba 28, 2023 alipokuwa akifunga rasmi Maonesho ya Utalii Kusini yaliyofanyika katika Viwanja vya Kihesa Kilolo, Mkoani Iringa.

Aidha, Kigahe amewakumbusha wawekezaji wa ndani kuwekeza katika Mkoa wa Iringa kwa kujenga hoteli zenye hadhi ya nyota tano na kutoa huduma nzuri kwa ajili ya kupokea wageni wengi zaidi.

Aidha ,Naibu Waziri amevutiwa na kauli mbiu ya Maonesho ya Mwaka huu 2023 isemayo "Mwelekeo mpya wa uwekezaji" kwani ni kauli yenye tija na kuwakumbusha wawekezaji katika maeneo yote ikiwemo sekta ya utalii kutimiza malengo waliyojiwekea.

Kigahe pia amepongeza maandalizi ya maonesho hayo yaliyoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Iringa Mhe. Halima Dendegu kwa kishirikiana na waratibu mbalimbali kutoka Mikoa yote ya Nyanda za Juu kusini.

Vilevile, amebainisha kuwa zaidi ya bilioni 16 zimewekwa kwa ajili ya kukuza utalii wa karibu kusini kupitia maonesho hayo ili kuweza kutengeneza mahusiano mazuri na watalii.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Iringa Mhe.Halima Dendego amesema kuwa katika Maonesho hayo walitarajia kupata waonyeshaji 100 lakini mwitikio umeleta waonyeshaji 110 na washiriki zaidi ya 800 kwa mwaka huu pamoja na mashindano ya magari.

Aidha, Dendego amesema Mkoa huo unaendelea kuboresha miundombinu ya uwanja wa ndege utakaoweza kubeba aina zote za ndege na kujenga Kituo cha Utalii na Utafiti.





# Vijana na Wananchi changamkieni fursa za ufanyaji biashara na uwekezaji katika mikoa yenu





Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe.Exaud Kigahe (Mb.) amewahimiza vijana na wananchi kwa ujumla kuchangamkia fursa za biashara na uwekezaji zilizopo nchini ili kuongeza ajira ,Pato la Taifa na kukuza uchumi wa Nchi.

Kigahe ameyasema hayo alipokuwa akifunga Kongamano la Biashara na Uwekezaji la JIONGEZE lililofanyika jijini Mbeya Oktoba 29, 2023 ambalo limefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kuhamasisha vijana na wananchi kuchangamkia fursa za biashara na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Mbeya na limewavutia wawekezaji wengi wa ndani na nje ya nchi.

Aidha, Kigahe amebainisha kuwa Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ikiwemo kianzisha Kitengo cha Uwekezaji, Viwanda na Biashara katika kila Halmashauri nchini na imezindua Dirisha la kielektroniki la kuwahudumia wawekezaji ambalo litawezesha wawekezaji kupata taarifa mbalimbali za uwekezaji nchini na kupata vibali na leseni kwa njia ya mtandao.

Vilevile, Kigahe amewapongeza WASAFI Group kwa kuanzisha Kongamano hilo, akisema kuwa kongamano hilo ni jukwaa muhimu la kuelimisha wananchi kuhusu fursa za biashara na uwekezaji zilizopo Nchini.

Kongamano la biashara na uwekezaji la JIONGEZE lilihusisha washiriki kutoka maeneo mbalimbali nchini, ikiwa ni pamoja na wawekezaji, wafanyabiashara, wajasiriamali na viongozi wa Serikali.





# Atakayekwamisha Wafanyabiashara ni adui namba moja wa Serikali

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Dkt. Hashil Abdallah amesema Afisa yeyote wa Serikali atakayekwamisha ufanyaji biashara, uwekezaji au uanzishwaji viwanda nchini ni adui namba moja wa Serikali na atachukuliwa hatua za kisheria.

Vilevile, Ametoa wito kwa watendaji hao kuwezesha uwekezaji, ufanyaji biashara, uanzishaji viwanda na kuhakikisha kila mwekezaji anapata anachostahili kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

Dkt. Abdallah ameyasema hayo Septemba 25, 2023, wakati akiongoza Kamati Maalum ya Katibu Mkuu Kiongozi inayojumuisha Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Fedha, Mipango na Uwekezaji, Kilimo na Katibu Tawala Mkoa wa Kagera walipotembelea Kiwanda hicho kuona hali ya uwekezaji na kutatua changamoto walizonazo.

Aidha, Dkt. Abdallah amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan ameweka Sera na Mazingira wezeshi katika ufanyaji biashara uwekezaji na uanzishaji wa viwanda ili kuiwezesha Tanzania kujitosheleza katika mahitaji ya bidhaa muhimu na kuuza ziada nje ya nchi na kutimiza malengo ya Tanzania kuilisha Dunia.

Akifafanua zaidi, Amesema Serikali imeanza kutimiza malengo hayo kwa kuanza na Sekta ya Sukari ambapo Kiwanda cha Sukari cha Kagera kinauwezo wa kuzalisha tani 150,000 kwa mwaka katika 2023/2024 na kinapanga kuzalisha tani 300,000 kwa mwaka kitakapokamilisha upanuzi wa awamu ya nne na hivyo kuchangia kuifanya Tanzania kutokuagiza sukari nje ya nchi, kuongeza ajira na pato la taifa hususan fedha za kigeni.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Kagera Bw. Tobi Nguvilo amesema uongozi wa Mkoa huo uko tayali kumlinda, kumtunza, kumsaisia na kuhakikisha hakwami kwa jambo lolote Mwekezaji wa Kiwanda cha Sukari cha Kagera kwa kuwa Mkoa huo unakitegemea kiwanda hicho kwa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii kwa kuajiri wananchi 115,000 kutoka Mkoani humo pamoja na utoaji wa huduma bora za shule na hospitali.

Vilevile, Mwenyekiti wa Chama cha Wazalishaji Sukari na Mmiliki wa Kiwanda cha Sukari Kagera Bw.Self Ally Seif amesema anaungana mkono juhudi za Serikali katika kuwawezesha wawekezaji ili kutimiza dhamira ya kuiwezesha Tanzania kuilisha Dunia kwa kuanza na Sekta ya Sukari inayotoa ajira nyingi na kuongeza pato la taifa zikiwemo fedha za kigeni.

## HABARI PICHA: ZIARA YA KAMATI MAALUM YA KATIBU MKUU KIONGOZI KIWANDA CHA SUKARI KAGERA

Kamati Maalum ya Katibu Mkuu Kiongozi ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Dkt. Hashil Abdallah inayojumuisha Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha Dkt. Natu Mwamba na Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Bw. Gerald Mweli, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera Bw Tobi Nguvilo Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari Prof. Kenneth Bengesi pamoja Mwenyekiti wa Chama cha Wazalishaji Sukari na Mmiliki wa Kiwanda cha Sukari Kagera Bw.Self Ally Seif wakitembelea sehemu za uzalishaji sukari, shule ya watoto, hospitali na mashamba wakati wa ziara yao katika Kiwanda cha Sukari cha Kagera Septemba 25, 2023 Mkoani Kagera kwa lengo la kujifunza na kuona hali ya uwekezaji katika Kiwanda hicho.











# HABARI PICHA

Kamati Maalum ya Katibu Mkuu Kiongozi ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Dkt. Hashil Abdallah inayojumuisha Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha Dkt. Natu Mwamba na Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Bw. Gerald Mweli, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera Bw Tobi Nguvilo wakiwa katika mazungumzo na Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mhe. Fatma Mwasa kuhusu maendeleo ya Mkoa huo Septemba 26, 2023 baada ya ziara ya kutembelea Kiwanda cha Sukari cha Kagera mkoani humo.







Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Dkt. Hashil Abdallah akiongea na Wafanyakazi wa Wakala wa Vipimo(WMA) Mkoa wa Kagera kuhusu kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma kwa umma Septemba 26, 2023 baada ya ziara ya kutembelea Kiwanda cha Sukari cha Kagera mkoani humo.











# Taasisi za Udhibiti zaelekezwa kuweka Mazingira Wezeshi ya Ufanyaji Biashara nchini

Taasisi za Udhibiti zimeelekezwa kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara nchini ikiwa ni jukumu kuu na la msingi ili kutatua kero za wafanyabiashara na wawekezaji kwenye sekta mbalimbali badala ya kuwa kikwazo na endapo kuna sheria, kanuni na taratibu zenye mikinzano zirekebishwe.

Wito huo umetolewa na Dkt. Hashil Abdallah, Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, alipokuwa akifunga Kikao kazi kilichohudhuriwa na Taasisi za Udhibiti Septemba 15, 2023 Morogoro ambapo Kikao hicho kiliratibiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Dkt. Abdallah amesema kuwa Taasisi za Serikali zinatakiwa kuzungumza kimifumo hasa katika maeneo yanayohusiana kiutendaji ili kumsaidia ambaye anataka kufanya baishara au kuwekeza nchini na kupata huduma kwa kasi kwakuwa uchumi wa nchi unakuwa kwa kutegemea mazingira bora ya ufanyaji biashara nchini na kuchochewa kuanzia ngazi ya Taasisi.

Ameendelea kusema kuwa Wizara kupitia Taasisi zake itaendelea kukutana mara kwa mara na wadau wa biashara ili kupokea changamoto zao pamoja na kuwapatia mrejesho wa hatua mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali.

kuboresha sekta ya biashara. Dkt. Abdallah amesisitiza kuwa ili kufanikisha utekelezaji wa azma ya Serikali ya Awamu ya Sita Wizara ya Viwanda na Biashara inatekeleza maono hayo kwa vitendo kwa kufanya mapitio ya Sera zake hususan Sera Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 ambayo kwa sasa iko katika ngazi ya Baraza la Mawaziri ambapo mapitio ya Sera hiyo yamezingatia wakati wa sasa wa ufanyaji biashara, mabadiliko ya sayansi na teknolojia pamoja na malengo ya Jumuiya mbalimbali za Kikanda na Kimataifa ambazo Tanzania imeridhia kuwa mwanachama.







# TBPL Zalisheni kibiashara na kwa Kasi viuatilifu hai

Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.) amekitaka Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibaolojia Tanzania (TBPL) kuzalisha kibiashara viuatilifu hai (Biopesticides) kwa kasi kwa ajili ya kupambana na wadudu waharibifu katika mazao ya kilimo wakati wa msimu wa mvua ujao.

Ameyasema hayo Septemba 21, 2023 akiwa na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Lugano Wilson wakati wa Mkutano na Waansishi wa Habari kuhusu maendeleo ya kiwanda cha TBPL uliofanyika kiwandani hapo, Kibaha mkoani Pwani.

Aidha, Amesema Wizara yake kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imepanga kuunganisha utekelezaji wa Mradi wa BBT na bidhaa zinazozalishwa na TBPL hususani viatilifu hai visivyo na kemikali vilivyopata ithibati ili kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa na Programu hiyo katika soko la ndani na nje ya nchi.

Dkt. Kijaji amebainisha kuwa viatilifu hai vilivyofanyiwa majaribio na kithibitishwa na TARI na kupatiwa cheti cha usajili na Mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA) ni rafiki kwa watumiaji na mazingira, vinaongeza thamani ya mazao katika soko na ni chanzo cha soko la wageni.

Dkt. Kijaji pia amesema kuwa Kiwanda hicho kimefanikiwa kuuza lita 272,444 za dawa ya viuadudu katika nchi 7 za Afrika ambazo ni Kenya, Angola, Niger, Botswana, Namibia, Eswatini na Msumbiji na ni bidhaa ya tano katika bidhaa 10 zinazotarajiwa kuuzwa katika soko la Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA).

Aidha, Ameelezea kuwa Wizara yake kupitia Shirika lake la NDC, TAMISEMI, Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha ziko katika hatua za mwisho za kuhuisha Mkataba wa ununuzi wa dawa za viuadudu vinavyozalishwa na TBPL ili kutimiza lengo la Serikali katika kutokomeza ugonjwa wa malaria nchini.

Naye, Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) Dkt. Nicholaus Shombe amesema Kiwanda cha kipekee Barani Afrika kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 6 za bidhaa za kibailojia zisizo na kemikali kwa mwaka ikiwemo viuadudu vya kuua viluwiluwi wa mbu wanaoeneza ugonjwa wa malaria na magonjwa mengine yanayoambukizwa na mbu, viatilifu hai vya kuua wadudu waharibifu kwenye mazao na mbolea hai.







# Wafanyabiashara watakiwa kuhakikisha Bidhaa zinakaguliwa na TBS kabla ya matumizi

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe.Dkt.Ashatu Kijaji ametoa wito kwa waagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi kuhakikisha bidhaa hizo zinakaguliwa na wenye Viwanda vya ndani kuhakikisha bidhaa zinakaguliwa na Shirika la Viwango Tanzania(TBS) kabla ya matumizi ili kulinda afya ya Watanzania.



Ametoa wito huo Septemba 18/09/2023 alipotembelea TBS kuona jinsi maabara za TBS 4 kati ya 9, ikiwemo maabara ya chakula, ngozi, nguo na kemia zinavyofanya kazi na kusikiliza changamoto zilizopo ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake katika Taasisi zote zilizopo chini ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023-2024 .

Aidha, Dkt. Kijaji ameridhishwa na utendaji kazi wa TBS na kuitaka ifanye kazi kwa kushirikiana na Taasisi zingine ili kurahisisha utendaji kazi kwa kuhakikisha Watanzania wanatumia bidhaa bora na salama kwa afya zao.



Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu Bw. Lazaro Msasalaga amesema TBS ina maabara tisa (9) zenye vifaa vya kisasa, wataalamu wa kutosha na zina ithibati kimataifa inazozitumia kupima ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini na zinazoingia kutoka nje ya nchi.

Akitaja maabara hizo, Bw. Msasalaga amesema Maabara hizo ni Maabara ya Kemia, Maabara ya Uhandisi Ujenzi, Maabara ya Uhandisi Mitambo, Maabara ya Uhandisi Umeme, Maabara ya Kemia ya Chakula, Maabara ya Mikrobiolojia, Maabara ya Pamba, Nguo na Ngozi, Maabara ya Ugezi na Kituo cha Teknolojia ya Ufungashaji.

# Kampuni za Wazawa zatakiwa kufanya Biashara kwa uadilifu na weledi







Serikali imeyataka Makampuni ya Wawekezaji Wazawa ambao wamesaini mikataba ya uchimbaji wa makaa ya mawe Mchuchuma kufanya biashara kwa uadilifu, weledi na juhudi ili kifikia malengo yanayo kusudiwa, kuongeza ajira na pato la Taifa hususani dola za marekani.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Viwanda na Biashara Dkt. Ashatu Kijaji Septemba 12, 2023 wakati wa hafla ya utiaji Saini wa Mikataba ya uchimbaji wa makaa ya mawe yaliyopo Ludewa mkoani Njombe kati ya wawekezaji wa ndani na Shirika la Taifa la Maendeleo, ambapo amesema baada ya miezi sita wawekezaji ambao hawajaanza kufanya shughuli za uchimbaji watanyang’anywa leseni.

Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Dkt. Lugano Wilson amesema uchimbaji wa makaa hayo ya mawe yatawezesha upatikanaji wa nishati muhimu na ya uhakika kwa uendeshaji wa viwanda nchini na maendeleo ya sekta hiyo kwa ujumla.

Naye Kamishina wa Madini na Mjumbe wa Bodi ya NDC Dkt. Abdulrahman Mwanga amesema mradi huo utaenda kuzalisha makaa ya mawe tani 30,000 kwa mwezi, huku wawekezaji hao wakisema watafanya kazi kwa muda uliopangwa ili kifikia malengo yaliyokusudiwa katika mradi huo.

Naye Mkurugenzi Mwendeshaji wa NDC Dkt. Nicolaus Shombe amesema Makampuni ya wawekezaji wazawa matano yamesaini mikataba hiyo na kukabidhiwa leseni ya uchimbaji na NDC ambayo ni Kindaini Company Limited, Chusa Mining Company Limited, Sheby Mix Investment Limited, Nipo Engineering Company Limited na Cleveland Mine and Service Company Limited.






# Wakulima ongezeni uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta ya kula





Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe Dkt Ashatu Kijaji(Mb.) ametoa wito kwa Watanzania kuongeza uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta ya kula hususan alizeti kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya viwanda vya uzalishaji wa mafuta ya kula nchini na kupunguza changamoto ya upatikanaji wa malighafi hiyo kwa uzalishaji wa mafuta ya kula kwa mwaka mzima.

Dkt. Kijaji ameyasema hayo Septemba 12, 2023 alipofanya ziara katika Kiwanda cha mafuta ya kula ya Korie na Sundrop pamoja na sabuni cha Wilmar Tanzania Limited, na Kiwanda cha kutengeneza kamba za plastik na ngazi cha Akberalis Hardware & Electric Limited (Dar Ropes) vilivyopo jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujionea shughuli za uzalishaji na kusikiliza changamoto.

Akiwa katika Kiwanda cha mafuta ya kula ya Korie na Sundrop pamoja na sabuni cha Wilmar Tanzania Limited, Dkt. Kijaji amewahakikishia Watanzania kuwa Kiwanda hicho kinaagiza mafuta ghafi na kuyachakata kupata mafuta ya kula na mabaki hutengenezwa sabuni. Bidhaa hizo huuzwa katika soko la ndani na nje hususani katika soko la EAC na SADC.

Akiwa katika Kiwanda cha kutengeneza Kamba za Plastik na Ngazi cha Akberalis Hardware & Electric Limited (Dar Ropes), Dkt. Kijaji amewashauri Watanzania kununua na kutumia bidhaa zinazalishwa nchini ili kuendelea kuzalisha ajira na kukuza pato la Taifa hususani fedha za kigeni.







# Serikali inaendelea kuilea Sekta Binafsi

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt Ashatu Kijaji(Mb.) amesema Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini ili kuiwezesha sekta binafsi kuongeza uzalishaji zaidi.

Waziri Kijaji ameyasema hayo Septemba 13, 2023 akiwa na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara Dkt. Lugano Wilson alipokutana na kuzungumza na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) Bw. Obinna Anyalebeche, ujumbe wake katika Ofisi ndogo za Wizara, jijini Dar es Salaam.

Aidha, amekipongeza Kiwanda hicho kwa kuendelea kuongeza uzalishaji wa bidhaa kupitia viwanda vyao vilivyopo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Kilimanjaro.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni SBL Bw. Obinna Anyalebeche ameishukuru Serikali kwa kuendelea kiilea sekta binafsi ili kuhakikisha wanazalisha zaidi na kulipa kodi stahiki kwa Serikali.

Aidha, Bw. Anyalebeche ameainisha mpango wa kiwanda hicho kuhakikisha wanapata malighafi hapa nchini na kuwahakikishia wakulima soko katika mazao yanayohitajika kuzalisha bidhaa zao





Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt Ashatu Kijaji(Mb.) akiwa na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara Dkt. Lugano Wilsonamekutana na kuzungumza kuhusu upatikanaji wa Barcode kwa wajasliamali kwa urahisi na Mtendaji Mkuu wa Global Standards (GS1)Tanzania Bi Fatma Kange Septemba 13, 2023 katika Ofisi ndogo za Wizara, jijini Dar es Salaam.

# FCT Inatoa maamuzi ya rufaa za mashauri ya ushindani na mashauri ya soko





Mkurugenzi wa Maendeleo ya Viwanda Dkt. Lugano Wilson akizungumza kwa Niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara Dkt. Ashatu Kijaji baada ya kupokea Taarifa ya Utendaji kazi wa Baraza la Ushindani (FCT) kutoka kwa Msajiri wa FCT, Mhe. Renatus Rutta, 11/09/2023 katika ofisi za Baraza hilo jijini Dar es Salaam.

Baraza la Ushindani au kwa lugha ya Kiingereza Fair Competition Tribunal (FCT) ni chombo huru cha kimahakama kilichoanzishwa na Serikali chini ya Sheria ya Ushindani Namba 8 ya mwaka 2003 (Fair Competition Act, No. 8/2003).

Madhumuni ya kuanzishwa Baraza hilo ni kuwa chombo maalumu cha kimahakama kitakachopokea, kusikiliza na kuamua kwa haraka rufaa zitokanazo na mashauri ya ushindani na udhibiti wa soko yatokanayo na maamuzi yanayofanywa na Tume ya Ushindani FCC na Mamlaka za udhibiti ambazo ni EWURA, TCAA TCRA, LATRA NA PURA.



# Taasisi zote zinazotoa huduma kwa wateja kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo wadogo

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb.) amezitaka Taasisi zote za umma ambazo hutoa huduma kwa wateja kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo wa madini kwa lengo la kuwasaidia wachimbaji hao kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na weledi mkubwa ili kuepukana na uharibifu wa Mazingira. Kigahe ameyasema hayo Septemba 22, 2023 alipokuwa akishiriki Kikao kazi cha watoa huduma za leseni zinazohusiana na uchimbaji na uwezeshaji mitaji katika ukumbi uliopo katika Viwanja vya Maonesho ya Sita (6) ya Teknojia ya Madini Geita.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb.) akikagua ujenzi wa Ofisi ya Machinga Mkoa wa Geita Septemba 22, 2023 ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa milioni 10 kwa ajili ya ujenzi huo wakati wa Siku Maalum ya Watoa Huduma/Leseni zinazohusiana na Madini na Uwezeshaji Mitaji katika Maonyesho ya Sita ya Teknolojia ya Madini yanayofanyika mkoani Geita.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb.) akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Geita Mhe. Cornel Magembe ametembelea Soko Kuu la Dhahabu la Geita Septemba 22, 2023 wakati wa Siku Maalum ya Watoa Huduma/Leseni zinazohusiana na Madini na Uwezeshaji Mitaji katika Maonyesho ya Sita ya Teknolojia ya Madini yanayofanyika mkoani Geita.





# Serikali haitambui kuwa Gunia ni Kipimo - Mhe-Kigahe

Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara Mhe Exaud Kigahe amesema kuwa Serikali haitambui kuwa Gunia ni kipimo bali itambulike kuwa ni Kifungashio kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo (The Weights and Measures Act (Amendment) Order, G.N. No. 725 of 2018,) jedwali la 10 chini ya kifungu cha (2) (b) cha Jedwali hilo, ambacho kinasema mazao ya mashambani yatafungashwa kwa uzito usiozidi kilogramu 100.

Mhe.Kigahe ameyasema hayo Septemba 6,2023 Bungeni Jijini Dodoma alipojibu swali la Mhe. Husna Sekiboko lililolenga kutaka kujua kama kwa mujibu wa Sheria Serikali inatambua gunia kuwa kipimo au kifungashio.

Aidha Naibu Waziri Kigahe ametoa wito kwa wadau wote kuepuka matumizi ya gunia kama kipimo kwani kwa kufanya hivyo ni kukiuka sheria ya Vipimo.

Vilevile Mhe. Kigahe amewataka wakulima wa mazao ya mashambani kuendelea kujiunga kwenye vyama vya msingi pamoja na kuuza mazao yao kwenye masoko ambayo Serikali imeelekeza Wakala wa Vipimo kupeleka Mizani kwa ajili ya upimaji wa mazao hayo.

# Serikali kuendelea kuhamasisha uwekezaji na uendelezaji wa viwanda Nchini-Mhe.Kigahe



Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara Mhe Exaud Kigahe amesema kuwa Serikali inaendelea na juhudi za kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vipya na uendelezaji wa viwanda vilivyopo katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi hususani Viwanda vya kuchakata mazao ya Mifugo na Uvuvi vikiwemo viwanda vya Nyama na Samaki katika Mkoa wa Rukwa na mikoa mingine nchini.

Mhe.Kigahe amebainisha hayo Septemba 8,2023 Bungeni Jijini Dodoma alipojibu swali la Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata linalotaka kufahamu kuwa ni lini Serikali itaviendeleza viwanda vya nyama na samaki mkoani Rukwa.

Aidha, Naibu Waziri huyo amesema kuwa Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeweka nguvu kubwa katika unenepeshaji wa mifugo pamoja na ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba, kutenga na kuboresha maeneo ya kukusanyia samaki (collection Centers) pamoja na minada ya mifugo ili kukidhi haja ya upatikanaji endelevu wa malighafi bora ya viwanda vya nyama na samaki nchini.

Vilevile Mhe.Kigahe ametoa rai kwa wavuvi na wafugaji kuviuzia malighafi viwanda vya ndani ili viweze kukidhi mahitaji yake.





# Wakandarasi Ongezeni Kasi ujenzi wa Jengo la TIRDO

Naibu Waziri Wizara ya Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb.) amewataka wakandarasi wanaojenga na kusimamia ujenzi wa jengo la Ofisi la Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO) kuongeza kasi ya ujenzi ili likamilike kwa wakati uliopangwa.

Ameyasema hayo Septemba 26, 2023 alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Ofisi hizo jijini Dar es salaam.

Aidha, Kigahe amesema kuwa Wizara inafahamu kuna changamoto zinazojitokeza hivyo amewaomba watumie fedha zilizotolewa kuboresha vitu vinavyowezekana ndani ya bajeti, na yale yanayoshindikana kuwe na sababu za kujitoshekeza.

Kigahe pia amewapongeza kwa hatua iliyofikiwa kwa sasa ikilinganishwa na hatua aliyoikuta katika ziara yake ya awali aliyoifanya.





# UJENZI WA JENGO LA CBE DAR-ES-SALAAM

Naibu Waziri Wizara ya Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe ameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa jengo la Metrology Annex unaendelea katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Kampasi ya Dar es Salaam.

Hayo yamebainishwa wakati wa ziara ya kikazi iliyofanyika tarehe 26 Septemba, 2023 ambapo ilielezwa kuwa jengo hilo litagharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 22.4, litakapokamilika na litakuwa la ghorofa 10.













# Serikali inaweka Mazingira Bora na Wezeshi kwa Wajasiliamali Wadogo wadogo

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah amesema Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kuweka mazingira bora na wezeshi yanayowasaidia wajasiliamali wadogo wadogo kuboresha bidhaa na kuongeza thamani mazao ya kilimo ili ziweze kukidhi soko la ushindani ndani na nje ya Nchi.

Dkt. Abdallah ameyasema hayo Septemba 26,2023 wakati akifunga warsha ya siku moja iliyokuwa ikijadili namna bora ya kuwekeza katika sekta ya kilimo cha chakula kwa maendeleo endelevu ya nchi iliyoandaliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya kiuchumi la Mennonite (MEDA) iliyofanyika katika Hoteli ya Coral Beach, jijini Dar es salaam.

Alisema kuwa kuimarisha uzalishaji wa kilimo, kutoa teknolojia ya kisasa, kukuza ukuaji wa ujasiriamali wa kilimo miongoni mwa wakulima wadogo na wafugaji pamoja na kuongeza maeneo ya umwagiliaji ni maeneo muhimu katika kuboresha kilimo nchini Tanzania.

Vilevile, aliipongeza MEDA Tanzania kwa kujitolea kwake kuendelea kuunga mkono maendeleo ya ujasiriamali nchini Tanzania, hasa kupitia utekelezaji wa miradi ya Kuimarisha Mnyororo wa Thamani wa Biashara Ndogo (SSBVC) na Wanawake Wajasiriamali kukuza Uchumi wa Kijani (FEGGE).

Kwa upande wake Mwakilishi Mkaazi wa MEDA Mussa Lubango, alisema lengo kuu la kuwepo kwa warsha hii ni kuwainua wakulima wadogo na wa kati katika sekta ya uchumi na maendeleo endelevu

Aidha, ametoa Pongezi kwa Serikali kupitia kwa Wizara husika kwa kutupa ushirikiano mzuri na kuwezesha warsha hii kufanyika nchini kwani tunaiona Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji wa chakula katika ukanda wa Afrika na Mashariki ya kati.



# Watumishi watakiwa kurudi na ushindi mnono mashindano ya SHIMIWI 2023

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb.) amewata watumishi wa Wizara hiyo kuhakikisha wanarudi na ushindi mnono watakaporejea Dodoma baada ya Michezo ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) kufikia tamati.

Kigahe ameyasema hayo Septemba, 28, 2023 Mkoani Iringa alipokuwa akizungumza na watumishi wa Wizara hiyo walioshiriki katika mashindano ya SHIMIWI yanayotarajiwa kuanza 29 Septemba, 29, 2023.

Aidha, Kigahe amewataka wachezaji washiriki michezo hiyo kikamilifu kwa kuwa inasaidia katika kuongeza uhusiano mzuri baina ya watendaji wa Serikali pamoja na kuimarisha afya za watumishi.

Kigahe pia alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuunga mkono michezo inayosaidia kuongeza uhusiano mzuri baina ya watendaji wa Serikali huku akiwataka kufanya vizuri kwa manufaa ya Taifa .

Kwa upande mwingine Kigahe aliwashukuru baadhi ya wadau walioshiriki katika kuishika mkono Timu hiyo ya Wizara katika mashindano hayo huku akiwaomba na wadau wengine kujitokeza kuwashika mkono katika mashindano yajayo.

"Vifaa hivi ambavyo tutavitumia katika michezo vimetolewa na Benki ya NMB na Barbers Limited, pia tunatambua michango ya taasisi za SIDO, FCC na WMA wamesaidia sana kwenye uratibu wa mambo mbalimbali pale walipohitajika". Amesema Kigahe

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na



Biashara Dkt. Hashil Abdallah amemshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara Dkt. Ashatu Kijaji na kuwataka wachezaji kucheza vizuri kwani mashindano ya sasa ni tofauti na mwaka uliopita hivyo kama Wizara wanatarajia kila timu na kila mechi kuingia na jezi mpya.

Amesema kuwa kupitia sekta ya Michezo wizara itakwenda kuiunganisha nchi katika sekta ya Biashara baada ya kuwa na watumishi wenye afya njema pamoja na nidhamu njema yenye ustawi, ari na hamasa kubwa.


WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
SHIMIWI-2023
KUVUTA KAMBA-WANAWAKE
FULL TIME
2-0
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII
30 Septemba 2023
viwandanabiashara
www.viwanda.go.tz


WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
SHIMIWI-2023
KUVUTA KAMBA-WANAWAKE
FULL TIME
1-1
29 Septemba 2023
viwandanabiashara
www.viwanda.go.tz


WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
SHIMIWI-2023
KUVUTA KAMBA-WANAUME
FULL TIME
2-0
29 Septemba 2023
viwandanabiashara
www.viwanda.go.tz


WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
SHIMIWI-2023
KUVUTA KAMBA-WANAWAKE
FULL TIME
2-0
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII
30 Septemba 2023
viwandanabiashara
www.viwanda.go.tz


FULL TIME
1-0
WIZARA YA MAJI
29 Septemba 2023
viwandanabiashara
www.viwanda.go.tz


pepsi
FULL TIME
1-0
WIZARA YA MAJI
29 Septemba 2023
viwandanabiashara
www.viwanda.go.tz


WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
SHIMIWI-2023
KUVUTA KAMBA-WANAWAKE
NMB
FULL TIME
2-0
30 Septemba 2023
viwandanabiashara
www.viwanda.go.tz


WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
SHIMIWI-2023
MATCH-DAY
KUVUTA KAMBA -WANAWAKE
VS
UWANJA: MKWAWA
MUDA: SAA 12:30 ASUBUHI
30 SEPTEMBA 2023
viwandanabiashara
www.viwanda.go.tz



Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Viwanda na Biashara
S.L.P 2996,40478 Dodoma,Tanzania Mji wa
Serikali Mtumba,Mtaa wa Viwanda.

Simu: +255 26 2963470
Nukushi: +255 26 2963117
Barua pepe:ps@mit.go.tz /gcu@mit.go.tz